**OFISI YA WAZIRI MKUUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**


**SHULE YA SEKONDARI YA UYUMBU,**

**S. L. P 151,**

**URAMBO.**

**09.12.2020.**

**Namba za Simu.**

**Mkuu wa shule: 0757297258/0658 642922**
**Makamu Mkuu wa shule: 0768 234782**


**KWA: ..........................................................**

**S. L. P 151,**

**URAMBO.**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI UYUMBU MWAKA 2021.</u>**

Uongozi wa shule ya sekondari Uyumbu unayo furaha kubwa kukupongeza kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha **KWANZA** katika shule hii. Shule ya sekondari Uyumbu ipo mkoa wa Tabora wilaya ya Urambo tarafa ya Ussoke Kata ya Uyumbu. Shule hii ipo umbali wa km 19 kutoka Ussoke na km 50 kutoka Urambo. Shule yetu ni ya mchanganyiko na shule ina wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha sita. Shule itafunguliwa siku ya Jumatatu tarehe **11.01.2021.** Wakati wa kupokelewa unatakiwa kuja na vitu vifuatavyo;

1. Fomu ya kujiunga na mahitaji ya shule.
2. Medical examination form.
3. Fomu ya kukubali kujinga na shule.
4. Historia ya mwanafunzi.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UYUMBU.**

..........................

**ELIAS S. SHILOTI**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
UYUMBU SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 151 URAMBO



Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

1. **SARE YA SHULE.**

**WASICHANA.**

- Sketi ndefu (2) linda box ya malinda rangi ya **DAAMU YA MZEE NDEFU** na kitambaa kiwe **kizito.**
- **Sketi zote za kushindia na za darasani ziwe ndefu.**
- Mashati meupe mawili (2) mikono mifupi.
- Nusu kanzu za darasani (2) nyeupe mikono mirefu zinazovuka makalio nzito au shati mikono mirefu (**kwa wanao vaa hijab).**
- Sweta moja la **RANGI YA DAMU YA MZEE.**
- T shirt 2 @ 6,000/= zinapatikana shuleni,
- Ushungi/Juba rangi ya **NJANO** ya kushindia kwa wanao vaa ushungi/Juba.
- Nusu kanzu za kushindia (2) rangi ya njano (kwa wanao vaa shungi.
- Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi,
- Soksi ndefu nyeupe,
- Tai ya **RANGI YA DAMU YA MZEE,**
- Sketi nyeusi mbili za marinda za kushindia,
- Vipodozi vya aina yoyote haviruhusiwi, wanja, piko,rangi za midomo/kucha n.k.
  **NB: WANAFUNZI WA KIKE HAWARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.**

**WAVULANA**

- Suruali (2) zenye marinda rangi ya RANGI YA DAMU YA MZEE sio **MODO** na kitambaa kiwe kizito CHINI SIZE 18,
- Mashati meupe (2) mikono mifupi,
- Sweta rangi ya RANGI YA DAMU YA MZEE.
- T-shirt 2 @ 6,000/=zinapatikana shuleni,
- Viatu vyeusi vya Kamba visigino vifupi na soksi nyeusi,
- Suruari ya kushindia nyeusi,
- Tai ya rangi ya DAMU YA MZEE.
- Mkanda wa ngozi mweusi.

**VIFAA VYA MICHEZO.**

- Bukta na t-shirt rangi ya blue (wavulana)
- Traksuti na t-shirt rangi ya blue (wasichana)
- Raba jozi moja.

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

## VIFAA VYA DARASANI

- Daftari kubwa angalau 10,
- Kalamu za wino za kutosha
- Kalamu ya risasi
- Kila mwanafunzi anashauriwa kununua kamusi ya kiingereza-kiswahili 1.

Tafadhali soma kwa makini maagizo / maelekezo hayo na kuyatekeleza kikamilifu. Vilevile tumeambatanisha fomu 03 kuanzia A, B na C nazo zinatakiwa kujazwa kabla ya mwanafunzi kuripoti sehemu husika.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UYUMBU.**



Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kufika shuleni:-

(a). Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

(c). Kushiriki kwa makini kufanya maandalio kama itakavyokuwa imepangwa (Preparation time).

(d). Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

(e). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii;

(f). Kuvaa sre ya shule, kikamilifu, wakati wote unapotakiwa;

(g). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

(h). Kutunza mali za Umma.

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a. Wizi.
b. Uasherati na ushoga.
c. Ubakaji.
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile: Uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli, n.k.
e. Kupigana au kupiga.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
g. Kudharau bendera ya Taifa.
h. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i. Kuoa au kuolewa.
j. Kutoa mimba.
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule.
l. Kukataa adhabu kwa makusudi.
m. Kuwa na **SIMU** ya mkononi.



Scanned with CamScanner
Scanned with CamScanner
Scanned with CamScanner

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI UYUMBU.**

**KIAMBATISHO (A)**

Nenda na fomu hii kwa mganga wa serikali akakupime na kukujazia

..... ................................

.............................................

..................................

Tarehe ........................

Mganga wa wilaya/mkoa,

S.L.P................................

.......................................

**MEDICAL CERTIFICATE:**

Jina la mwanafunzi.........................................................................................

1.Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona amepatikana na ugonjwa wa................................................na nimemtibu ipasavyo.

2.Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona na ugonjwa hawezi kusoma kwasababu ya.............................................................................................................................

...............................................................................................................................

3.Kwa wasichana tu, nimemwona ana mimba/ hana mimba.Tutakayemtilia mashaka tutampeleka hospitali kwa daktari wa hapa wilaya ya Urambo.

4.Afya yake kwa ujumla.

a) Kifua.......................................................................................
b) Macho...................................................................................
c) Masikio...................................................................................
d) Kilema chochote kitaje...........................................................
e) Akili........................................................................................
f) Mkojo (urine).........................................................................
g) Choo (stool)...........................................................................
h) Mimba...........................................................................................Sahi hi ya mganga......................................... Mhuri:

Tarehe...................................



Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

SHULE YA SEKONDARI UYUMBU,

S.L.P 151,

URAMBO.

## HISTORIA YA MWANAFUNZI: FOMU (B)

1. Jina la Mwanafunzi: ..............................................................
2. Tarehe kamili ya kuzaliwa: ................................
3. Jina la Baba: ..........................................................................
4. Jina la Mama: .........................................................................
5. Jina la Mlezi: ..........................................................................
6. Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi: ...............................................
7. Uhusiano wa Mlezi: ................................................................
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi (Mkulima, Mfanyakazi,Mfanyabiashara)..............................
9. Kama ni Mfanyakazi, kazi yake: ..................................................................
10. Kama Mkulima zao muhimu analotegemea: .................................................
11. Kama Mfanyabiashara, Biashara yake: ......................................................
12. Afya yake (Maelezo kama mwanafunzi anayomatatizo ya kiafya na hivyo anastahili huduma maalum) ..........................................................................................................
13. Madhehebu ya dini ya Mwanafunzi: ....................................
14. Jamaa, Ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya Mzazi/Mlezi;

| JINA KAMILI | UHUSIANO | ANUANI YAKE |
|---|---|---|
| 1) | | |
| 2) | | |
| 3) | | |

15. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:

    Mimi: ....................................................................Nathibitisha kuwa maelezo yaliyotajwa hapo juu ni sahihi.

    Anuani ya Mzazi/Mlezi: ....................................Tarehe: ...............................



Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI UYUMBU,**

**S.L.P 151,**

**URAMBO.**

**KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE: FOMU (C)**

1. Jina la mwanafunzi: ................................................................................

2. Jina la mzazi/mlezi: ................................................................................

Mimi ........................................................................................ nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Uyumbu, nakubali nafasi hii niliyopewa Umma wa Tanzania. Naamini kabisa nimetunukiwa nafasi hiyo ili niliendeleze kwa manufaa ya watanzania. Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa shuleni, nje na ndani ya darasa. Ili kutimiza shabaha hii ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa **BUSARA, MAARIFA, NIDHAMU YA HALI YA JUU** na **UTII** kwa viongozi wote kwa sharia na amri za shule. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi................................ Tarehe.......................................

Mimi ........................................................................ nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi........................................................................................ naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo na kushirikiana na shule na nitakuwa tayari kulipa gharama za uharibifu wowote utakaojitokeza wa mali za Umma/Shule utakaokuwa umefanywa na mtoto wangu.

Sahihi ya mzazi/mlezi ................................ Tarehe ....................................



Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner